



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA
KUADHIMISHA WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA OKTOBA 5 HADI 9, 2026

Dar es Salaam, 5 Oktoba 2026

Wiki ya Huduma kwa Wateja ni tukio linaloangazia umuhimu wa utoaji wa huduma bora kwa wateja na nafasi ya watoa huduma katika kujenga uhusiano mzuri na wateja. Maadhimisho haya yanatoa fursa kwa taasisi na mashirika mbalimbali kutafakari namna ya kuboresha huduma, kuongeza ubunifu na kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi na kuzidi matarajio ya wateja.

Kwa kutambua mchango na umuhimu wa wateja katika kuboresha Sekta ya Usafiri Ardhini, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inaungana na wadau wengine kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja kuanzia tarehe 5 hadi 9 Oktoba 2026, kwa kuzingatia kaulimbiu **“Extra Mile”**, yaani **“Kufanya Zaidi ya Kinachotarajiwa.”**

Kaulimbiu hii inatukumbusha kuwa, katika kuwahudumia wateja, tunapaswa kwenda hatua ya ziada kwa kutoa huduma bora, zenye ufanisi na zinazozingatia viwango vya kimataifa, huku tukizingatia misingi ya Uweledi, uadilifu, uwazi na uwajibikaji.

LATRA inatoa huduma zake kwa kuzingatia Mfumo wa Usimamizi wa **Ubora (Quality Management System)** na imepata Cheti cha Uthibitisho kwa Kiwango cha **Kimataifa ISO 9001**. Mfumo huu unalenga kumjali mteja na kuendelea kuboresha huduma zinazotolewa ili kufikia na kuzidi matarajio ya wateja, kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utendaji iliyopo.

Katika kutekeleza dhamira hiyo, LATRA inaendelea kutekeleza Sera ya Ubora kwa kumjali mteja na kuhakikisha huduma zinazotolewa kwa kuzingatia ubora, uwazi, uweledi, usawa, usahihi na kwa wakati. Aidha, Mamlaka inaendelea kuimarisha mifumo ya utoaji huduma, ikiwemo matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji, pamoja na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja mwaka huu, LATRA itaendelea kusikiliza maoni, mapendekezo na changamoto za wateja na wadau wake ili kubaini maeneo yanayohitaji maboresho na kuchukua hatua stahiki. Wasiliana nasi kwa kupiga simu bila malipo **0800 11 00 19/0800 11 00 20** au WhatsApp **0681 300 800** au kwa baruapepe info@latra.go.tz, au kupitia mfumo wa e-Mrejesho.

Imetolewa na;

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano